

Kuishi na Yesu Mfufuka

Na Askofu Lucas Luhigilo Mbedule

Ezekieli 37: 1 - 8

Utangulizi

Juma hili tunaadhimisha Pasaka yaani kufufuka kwa Yesu Kristo kutoka kifo. Nyuma ya kifo cha Yesu tunaona jinsi tawala tatu zilivyoungana katika kunyamazisha kazi na Utume wa Yesu. Tena tunaona jinsi haki inavyodhulumiwa na maandalizi ya kazi za kubambikiziwa kesi.

Tawala hizo 3 ni:

- Pilato aliwakilisha Serikali ya Rumi
- Herode aliwakilisha utawala wa Wayahudi
- Kayafa aliwakilisha dini ya Kiyahudi

Tunaona jinsi Shetani anavyoweza kutumia Serikali za kidunia na tawala za kidini kunyamazisha utume. Hata mashtaka ya Yesu yana sura mbili: La kwanza lilikuwa shtaka la kiserikali kwa kudaiwa kuzuia watu wasilipe kodi na kwamba anajiita Mfalme. La pili lilikuwa shtaka la kidini kwamba alikuwa anaponya watu siku ya sabato na kusema atabomoa hekalu na kulijenga kwa siku tatu.

Pasaka inatufanya tuone jinsi Shetani anavyoweza kutumia tawala na dini kuharibu kazi za Mungu na utume kwa kunyamazisha sauti ya unabii. Tena tunajifunza jinsi mtu mwenye nafasi au nguvu kiutawala au kifedha anavyoweza kupora haki za watu. Unaposikia makelele na mizozo ujue haki inaporwa. Lakini Yesu ameshinda dhuluma, dhambi na mauti tena tunaona Yesu ni mzima kwa kufufuka kutoka mautini. Hivyo kifo na dhambi hazina nguvu tena.

Tunaposoma Kitabu cha Nabii Ezekieli 37: 1 – 8 tunakutana na nguvu ya Mungu dhidi ya mauti. Mifupa iliyokuwa imekauka na bila ngozi Mungu anaipa uzima mpya na tunaona kumbe ufufuo upo tangu agano la kale. Mungu anatenda miujiza katika mashaka ya Ezekieli na watu wote. Mungu anaonesha alivyo na mamlaka dhidi ya kifo na mauti.

Wako watu wamekufa katika dhambi muda mrefu lakini miili yao ipo. Hawajafufuliwa. Wanafanya kazi za Mungu lakini wamekufa kwa kuwa hawako tayari kufufuliwa au kubadilishwa. Mungu anataka kutufufua kutoka dhambini na uovu ili tuwe wazima. Tatizo watu wengi wameng'ang'ania dhambi na hawako tayari kufufuliwa kuwa wapya. Ni kama mifupa katika bonde, ambayo haijafikiwa na uzima.

Mwaka 1982 Marehemu Askofu Dkt. Judah Kiwovele wa Dayosisi ya Kusini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) alituhumiwa kuwa anafukuza Wachungaji. Ikiwa ni hivyo swali likawa je, akifukuza Wachungaji atafanya kazi na nani? Askofu Kiwovele akajibu: “Mimi sifukuza Wachungaji, ninachofanya ninaifukuza dhambi iliyo ndani ya mtu, kwa bahati mbaya dhambi inapomtoka na kumkimbia nashangaa na Mchungaji wangu anakwenda iliko dhambi.”

Watu wengi wanaifuata dhambi na wanapenda kuishi katika dhambi. Mungu anataka kutufufua kutoka mawazo mabaya, maisha mabaya na matendo mabaya ili tubaki katika milki yake na tufufuliwe na Kristo, tuwe wapya. Bwana akubariki.

(Askofu Mbedule ni Mkuu wa Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Kanisa la iinjili la Kilutheri Tanzania
e-mail: mbedulelucas@gmail.com Simu: +255 769888 669)